**ALLIANCE FOR CHANGE AND TRANSPARENCY (ACT WAZALENDO)**

**OFISI YA KATIBU MKUU**
***(Party's Secretary General Office)***

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu waandishi wa habari,

Chama ACT Wazalendo, tumekuwa tukifuatilia kwa karibu sana mwendo wa bei za mafuta zinazotangazwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa kila Mwezi

Kwa muda wa miezi mitano (5) mfululizo kutoka mwezi wa Julai mpaka mwezi wa Novemba mwaka huu bei ya Mafuta Zanzibar imekuwa na ongezeko kubwa ukilinganisha maisha halisi na kipato cha Wazanzibari. Ni jambo ambalo halijawahi kutokea nchini kuwa na ongezeko kubwa la bei ya Mafuta kwa kipindi kifupi cha miezi mitano kama ilivyo sasa.

Ndugu Waandishi wa habari,

Kwa kipindi hichi cha miezi mitano Bei ya mafuta ya Petroli imepanda kutoka Shilingi 2700 kwa Mwezi wa Julai mpaka kufikia Shilingi 3187 kwa mwezi wa Novemba, ongezeko la shilingi 487 sawa na wastani wa asilimia 15.2. Kwa bei ya mafuta ya Dizeli yamepanda kutoka shilingi 2746 kwa mwezi wa Julai mpaka kufikia shilingi 3323 kwa mwezi wa Novemba, ongezeko la shilingi 577 sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 17.36 na bei ya mafuta ya Taa yamepanda kutoka shilingi 2921 kwa mwezi wa Julai mpaka kufikia shulingi 3300 kwa mwezi wa Novemba, ongezeko la shilingi 379 sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 11.48. Mchanganuo wa bei za mafuta zilizotangaazwa na ZURA kwa kipindi cha miezi mitano (5) kutoka mwezi wa Julai 2023 mpaka mwezi wa Novemba 2023 ni kama inavyoonekana hapo chini.

Vuga - Zanzibar, P.O. Box 105043,
Tel: +255 777 414 112 / +255 655 314 112
Email: info@actwazalendo.or.tz Website: www.actwazalendo.or.tz

| AINA YA MAFUTA | JULAI | AGOSTI | SEPT | OKT | NOV | ONGEZEKO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Petroli** | 2700 | 2970 | 2950 | 3001 | 3187 | **487** | **15.2%** |
| **Dizeli** | 2746 | 2843 | 3012 | 3282 | 3323 | **577** | **17.36%** |
| **Mafuta ya Taa** | 2921 | 2921 | 2921 | 2921 | 3300 | **379** | **11.48%** |

Ndugu Waandishi wa habari,

Chama cha ACT Wazalendo kinaona kwamba kupanda huku kwa kiwango kikubwa kwa bei ya mafuta nchini sio jambo la kawaida na linazidi kuathiri wananchi wa Zanzibar hasa wenye kipato cha chini. Athari hizi zinaonekana katika hali ya kawaida tu, katika kutazama maisha ya watu. Miongoni mwa athari hizo ni kama zifuatazo:-

1. **Mfumko wa Bei:** Ni wazi kwamba kupanda huku kwa bei za bidhaa za chakula na bei za bidhaa nyengine nchi kunatokana moja kwa moja na kupanda kwa bei za mafuta, huku Mamlaka zinazosimamia bei za bidhaa zikiwa kimya na kujifanya kutokujua sababu hizi za bei za bidhaa mbali mbali nchini, ukweli upo wazi kwamba mfumko huu wa bei katika bidhaa mbali mbali kunatokana na kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa hizo kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta. Ni wazi kwamba wafanyabiashara hujifidia gharama hizo za usafiri kwa kupandisha bei bidhaa zao.
2. **Wafanyabiashara wadogo wadogo kufunga biashara zao kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji:** Ni wazi kwamba kupanda huku kwa gharama za mafuta kunapelekea kufa kwa biashara ndogo ndogo, ambazo ukuaji wake unategemea mtaji usioyumba na wateja wa kila siku. Kupanda huku kwa bei za mafuta kunapelekea wafanyabiasha wadogo wadogo hasa wafanyabiasha wa bidhaa za kilimo kuengeza bei za bidhaaa hizo na kupelekea kupungua kwa wateja kutokana na kuengezeka huko kupanda kwa bei za bidhaa hizo.
3. **Kuengeza Mzigo Mkubwa wa Maisha kwa Wananchi:** Ni wazi kwamba kupanda huku kwa bei ya Mafuta nchini muathirika mkubwa anabaki kuwa mwananchi wa kawaida ambae atakuwa anapambana na kuzimudu gharama hizo za kununua bidhaa kama vile Vyakula vinavyozalishwa ndani na nje ya Zanzibar. Kupanda kwa gharama za usafiri wa kawaida na usafiri wa bidhaa, kupanda bei kwa vifaa vya ujenzi na

mahitaji mengine mbali mbali ambayo upatikanaji wake unategemea mafuta katika usafiri wake au uzalishaji wake.

**Wito wetu.**

1. ACT Wazalendo tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mapitio ya Mfumo wa uliopo wa uingizaji mafuta ya jumla (bulk supply) ambao una ukiritimba wa muda mrefu. Mfumo huo unapunguza ushindani na hivyo uwezekano wa kutumika vibaya na muagizaji pekee;
2. ACT Wzalendo tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuangalia upya mfumo wa kodi za Serikali katika Sekta ya Nishati na Mafuta Nchini ili kuweka unafuu kwa wananchi. Kwa mfano, katika miaka ya nyuma kulikuwa na Sera maalum ya kudhibiti bei ya mafuta ya taa kwa kuyaondolea kodi zote inapobidi;
3. ACT Wazalendo tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutazama upya gharama za uingizaji wa mafuta kutoka katika bandari ya Dar es Salaam kuja bandari ya Zanzibar, kuna uwezekano mkubwa kuwapunguzia wananchi mzigo huu mkubwa ambao wanaubeba.
4. ACT Wazalendo Tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwa na sehemu ya kuhifadhia mafuta kwa dharura yaani (Strategic Fuel Reserve Facility) ili kuruhusu mfumo wa kuagiza mafuta angalau kwa miezi mitatu ili kuondosha utaratibu huu wa kupandisha bei ya mafuta kiholela na kila baada ya mwezi, kwani jambo hili linaharibu kabisa mipango na bajeti na mipango ya wafanyabiashara na wananchi ambazo wanajiwekea kutumia katika mwezi husika. Matangi ya Mafuta ya Serikali ya Mtoni ambayo sasa yamekodishwa yalijengwa kwa madhumuni hayo. Hivyo, ni wakati kutafakari upya umuhimu wa jambo hilo.
5. Tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupunguza matumizi ya Serikali, ikiwemo magari na matumizi yasio ya lazima ili kufidia na kubeba ghrama hizi za ongezeko la bei ya Mafuta kwa kila mwezi.

**Ahsante sana kwa kunisikiliza**

**Salim A. Bimani,**
Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma,
Chama cha ACT-Wazalendo
11/11/2023

Vuga - Zanzibar, P.O. Box 105043,
Tel: +255 777 414 112 / +255 655 314 112
Email: info@actwazalendo.or.tz Website: www.actwazalendo.or.tz